



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJİ TUNDUMA

30/09/2023

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa kwenye tangazo hili kuomba nafasi za kazi ya mkataba wa miezi mitatu (03) ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

**WAKUSANYA USHURU (MAKARANI) - NAFASI 65**

**KAZI NA MAJUKUMU.**

1. Kukusanya Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia Mashine za Kielectronic za kukusanya Mapato (POS)
2. Kuhakikisha Fedha inayokusanya inapelekwa Bank katika akaunti za Halmashauri kwa wakati
3. Kuhakikisha Mapato yote yanayopaswa kukusanya na Halmashauri yanakusanya kwa usahihi
4. Kutunza kumbukumbu za Hesabu
5. Kutunza vizuri mashine za kukusanya Mapato (POS)
6. Kutoa na kuwasilisha taarifa za makusanyo ya kila siku kwa Halmashauri
7. Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na Msimamizi wake

**NB: MSHAHARA KWA MWEZI SHILINGI 200,000 (LAKI MBILI KWA MWEZI)**

Kuajiriwa wenye Elimu ya kuanzia Astashahada (Certificate) na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia simu janja (Smart phone), sababu Mapato yote ya Serikali yanakusanya kwa kutumia Mashine za Kielectronic za Kukusanya Mapato (POS) ambayo ina application sawa na simu janja. Aidha waombaji wenye sifa Zaidi ya zilizotajwa hapo juu maombi yao hayatafikiriwa

## MASHARTI YA WAOMBAJI KATIKA KAZI HII

1. Awe ni raia wa Tanzania
2. Awe amehitimu kidato cha Nne /sita
3. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali
4. Awe na Umri wa kati ya 18 - 45
5. Muadilifu asiye na Kasoro yoyote
6. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina mawili ya Wadhamini Watumishi wa Umma (Referees) na anwani zao sahihi na namba za simu.
7. Maombi yaambatane pamoja na nakala ya vyeti vyote kitaaluma, na Cheti cha kuzaliwa vya Mwombaji.
8. Awe na Kitambulisho cha Taifa / Namba ya NIDA
9. Awe tayari kupangiwa kituo chochote cha kukusanya Mapato ndani ya Mji wa Tunduma.
10. Awe Muaminifu katika kukusanya Mapato ya Serikali na kuhakikisha fedha ya Serikali haipotei.
11. Awe tayari kutij na kufuata maelekezo atakayopangiwa bila kuvunja misirgi ya Sheria ndogondogo za Halmashauri.

### JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya Mwombaji pamoja na namba ya simu na zitumwe kwa anuani ifuatayo;


**MKURUGENZI WA MJI,**

**S.L.P 73,**

**TUNDUMA.**

### TAREHE YA MWISHO YAKUPOKEA MAOMBI:

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/10/2023 sa 9:30 Alasiri

  
Belton Garigo

**MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MJI  
TUNDUMA**

KAIMU MKURUGENZI WA MJI